**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/472/LZ/2024/07**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000242**

**KATI YA**

**EMMANUEL FREDY MARWA ……...............................................MLALAMIKAJI**

**NA**

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA**
**MAZINGIRA MUSOMA (MUSOMA WSSA)………………………... MLALAMIKIWA**

---

**AMRI**

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA tarehe 15 mwezi Januari 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 15 mwezi Januari 2025, kwa madai kwamba Mlalamikiwa aamrishwe kumshirikisha Mlalamikaji katika usomaji dira na kusoma dira kila mwezi kuepuka malimbikizo ya ankara na kufanya deni kuwa kubwa. Mlalamikaji ni mkazi wa Machinjioni,Manispaa ya Musoma, Mkoa wa Mara.

Baada ya kupokea malalamiko tarehe 18 Septemba 2024, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (*EWURA (Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020)*) TS Na. 428/2020.

Mnamo tarehe 15 Novemba 2024, Mlalamikiwa aliwasilisha utetezi wake na kuiambia Mamlaka kwamba Mlalamikaji ni mteja wao mwenye akaunti namba A445D1112411 na mita namba 10929406. Mlalamikiwa anaendelea kueleza kuwa matumizi ya Mlalamikaji yako sawa na hakuna changamoto yoyote. Mlalamikiwa anaeleza zaidi kwamba kuhusu kumshirikisha wakati wa usomaji.

Mlalamikaji anapaswa kuwepo eneo husika lakini pia huwa anatumiwa ujumbe mfupi kupitia simu yake ya mkononi ikimtaarifu usomaji wake na kumuelekeza kuhakiki usomaji huo katika mita yake. Kikao cha usuluhishi kilifanyika tarehe 18 Disemba 2024, katika Manispaa ya Musoma, wakati wa kikao cha usuluhishi, Mlalamikaji alielezwa namna ambavyo Mlalamikiwa anavyowashirikisha wateja wake kwenye usomaji wa mita na pia kwa pamoja walihakiki taarifa za ankara na kuonekana ziko sawa.

Mlalamikaji akiwakilishwa na Robinson Wangaso wa EWURA CCC, Mkoa wa Mara, aliandika barua na kuifahamisha Mamlaka kwamba Mlalamikaji ameridhika na maelezo ya Mlalamikiwa na ameomba kuondoa malalamiko yake dhidi ya Mlalamikiwa. Barua hiyo ilipokelewa kwenye ofisi za EWURA-Kanda ya Ziwa tarehe 23 Disemba 2024. Hivyo basi, Mlalamikaji anaomba kuondoa shauri lake EWURA.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yaondolewe na kila upande utabeba gharama za uendeshaji wa malalamiko haya.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 15 mwezi Januari 2025.

..........................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**